**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

## KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu Maoni ya Kamati ya Uchumi juu ya mchakato mzima wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola Mtukufu mwenye kustahiki kushukuriwa na Viumbe vyote kwa kutujaalia amani, utulivu, uhai na afya njema tukaweza kukutana leo katika Baraza lako Tukufu kwa lengo la kujadili, na hatimae, kuipitisha Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, ili kuiruhusu Wizara kutekeleza kwa ufanisi Programu Kuu tatu (3) ilizojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi za pekee nazitanguliza kwake Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Taifa letu katika Uchaguzi uliofanyika Oktoba 2020. Ushindi aliopata Rais wetu ni uthibitisho tosha kuwa Wananchi wana Imani nae pamoja na Sera na Ahadi zake, na kwa kweli, Wazanzibari sasa wana shauku na hamu ya kuiona Zanzibar mpya yenye neema tupu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee kabisa, naomba kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuapishwa kwake kunathibitisha kuwa Taifa letu linaendeshwa kwa Misingi imara ya kikatiba inayozingatia usawa bila kujali rangi, kabila au jinsia. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amfanyie wepesi katika kuyatekeleza majukumu yake, AMIN!!

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa dhati kabisa, naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ni imani yetu kuwa viongozi hawa watamsaidia vizuri Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha malengo ya Serikali ya awamu ya 8 yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Uchumi, napenda kukushukuru kwa dhati kabisa, wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda niwapongeze Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu kwa juhudi wanazozichukua za kuwawakilisha wananchi wao, juhudi zao zimewawezesha Wananchi kujenga imani kubwa kwa Baraza Lako, nasi tunawaahidi kwamba tutaendelea kuwatumikia kwa dhati kama ambavyo walivyotuamini kutuchagua na kutuleta katika chombo hiki kwa lengo la kutetea maslahi yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Wajumbe wa Kamati ya Uchumi walifanya kazi kubwa ya kuipitia kwa kina Bajeti ya Fungu L02 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kufanya marekebisho madogo madogo. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo :-

1. Mhe. Shaaban Ali Othman – Aliyekua Mwenyekiti
2. Mhe. Sabiha Filfil Thani –Aliyekua M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hassan Hamad Omar – Mjumbe
4. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf – Mjumbe
5. Mhe. Juma Makungu Juma – Mjumbe
6. Mhe. Hamza Hassan Juma – Mjumbe
7. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Mjumbe
8. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu – Mjumbe

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi kwa karibu sana na makatibu wawili (2) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba niwatambue

1. Ndugu Asma Ali Kassim – Katibu
2. Ndugu Adam Maulid Simai – Katibu

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ya Uchumi imefanya kazi ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, siku ya tarehe 28/04/2021, kwa kuzingatia matakwa ya Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mujibu wa Bajeti inayozingatia matokeo yaani (PBB), Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Fungu Kuu moja la L02 na limepangiwa kutekeleza Programu kuu tatu (3) zenye Programu ndogo sita (6) ambazo kwa ujumla wake zinajumuisha shughuli na huduma zote zinazokusudiwa kutolewa na Wizara hii katika mwaka ujao wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajiwa kukusanya jumla ya Tsh 2,259,412,000 Bilioni kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Aidha, Wizara inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh 58,542,991,000 Bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara. Kati ya fedha hizo, Tsh 5,654,700,000 Bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida na Tsh 52,888,291,000 Bilioni ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima, sasa naomba nitoe maoni ya Kamati ya Uchumi kwa Programu Kuu za Wizara hii ambazo Kamati yangu imezitolea maelekezo na ushauri kama ifuatavyo:

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu hii ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imeundwa na Programu moja ndogo ya maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Programu hii inatekelezwa na Idara ya Maendeleo na Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Pamoja na Mafuta na Gesi). Aidha, lengo kuu la Programu Kuu hii ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu. Programu hii kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, imekadiriwa kutumia jumla ya Tsh 2,448,000,000 Bilioni.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ndio inayoshughulikia masuala yote ya udhibiti, ufatiliaji, na uendelezaji wa Mafuta na Gesi. Natoa pongezi kwa Wizara kwa kujipanga vizuri katika kuyasimamia masuala yote ya mafuta na gesi kwenye visiwa vyetu. Ni imani ya Kamati yangu kuwa Sera zitatayarishwa na kusimamiwa, Kanuni mbali mbali

zitatekelezwa, Mafunzo mbali mbali kwa jamii na watendaji yatatolewa, miongozo mbali mbali itatolewa na kadhalika, ili kufikia malego ya Wizara na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inasisitiza sana suala la tafiti. Naiomba Wizara ifanye Tafiti za kina katika masuala mazima ya Mafuta na Gesi ili kuipunguzia Serikali gharama, na kuleta matokeo chanya katika kufanikisha upatikanaji wa Mafuta na Gesi nchini. Aidha, naiomba Wizara kutoa mafunzo elekezi kwa watendaji ili kuwajengea uwezo wa kutatua changamoto mbali mbali zitakazojitokeza wakati wa kutekeleza majukumu yao, lakini pia kutaipunguzia Serikali gharama za kutafuta wataalamu wa nje na tutatoa watendaji watakaobobea katika masuala mazima ya Mafuta na Gesi.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi imeundwa na Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Rasilimali za Bahari. Programu zote hizi kwa pamoja

zinatekelezwa na Idara ya Uvuvi na Maendeleo ya Mazao ya Baharini pamoja na Idara ya Uhifadhi wa Bahari. Aidha, Programu Kuu hii ina lengo la kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya baharini kwa njia ya ufugaji. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu hii imekadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 2,259,412,000 Bilioni katika vyanzo mbalimbali vya mapato na kutumia jumla ya Tsh 54,321,906,000 Bilioni katika kutekeleza shughuli mbalimbali za programu hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Wizara kwa kutoa mafunzo kila mwaka kwa kamati zote 91 za Uvuvi nchini. Tunaiomba Wizara kuendelea kutoa mafunzo kwa kamati hizi na kuvifikia vikundi vyengine vinavyojishughulisha na uvuvi, ili kuleta tija na kuongeza kipato kwa wananchi wetu, ambao kwa asilimia kubwa wanajishughulisha na masuala ya uvuvi. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuchukua juhudi za ziada za kuvifikia vikundi mbali mbali, vijiji na wadau mbali mbali wa masuala ya Uvuvi ili kuzitatua changamoto za msingi zinazowakumba kwa dhumuni la kuongeza tija, ufanisi na kipato kwa Serikali na Wananchi, ukizingatia kuwa kwa asilimia kubwa Uvuvi ni shughuli kuu kwa Wazanzibari walio wengi. Halikadhalika, Kamati yangu inashauri Wizara kujikita

katika kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe faida na fursa zinazotokana na dhana nzima ya Uchumi wa Buluu.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa jukumu la msingi la Wizara hii ni kuimarisha ulinzi katika maeneo yetu ya bahari kwa kupiga doria za kutosha. Kamati imesikitishwa na mpango wa Wizara kujipangia kununua boti moja ya doria kwa mwaka wa fedha 2021/2022, idadi ambayo haiendani na kasi ya Uchumi wa buluu. Halikadhalika, boti zilizokuepo hazina uwezo unaoridhisha ambapo zina mashine yenye uwezo wa Horse Power (HP) 240, uwezo ambao ni mdogo sana na haukidhi sifa za boti za doria. Kamati inaishauri Wizara kununua boti za doria zenye nguvu zaidi ya Horse Power (HP) 800 ili kuimarisha ulinzi na doria pamoja na kwenda sambamba na kasi ya Uchumi wa Buluu.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ilivifikia vikundi vitano (5) vya kusarifu Mwani na imejipanga kuvifikia vikundi Kumi (10) kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa ajili ya kuvipatia mafunzo. Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Wizara kuona umuhimu wa kuongeza mafunzo kwa wakulima hao kwani tunaamini kuwa elimu na ujuzi ndio msingi wa maendeleo ya

sekta hii. Hata hivyo, Kamati inashauri vikundi hivyo viwezeshwe kwa kupewa vifaa vya kilimo cha mwani ili kuongeza tija na kuliendeleza zao la mwani.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imeingiwa na hofu juu ya maendeleo yasiyoridhisha ya Kampuni ya ZAFICO. Tangu kuundwa kwa Kampuni hiyo, Serikali imekua ikiiendesha kwa hasara, ukizingatia kiasi cha fedha ambazo Serikali kila Mwaka inawekeza kwenye Kampuni hii. Mpaka kufikia Machi mwaka huu, Kampuni imekusanya jumla ya Tsh 16,656,450 Milioni na imetumia jumla ya Tsh 1.43 Bilioni. Kamati inaiomba Serikali kuiangalia upya Kampuni hii kwa kujiridhisha uwezo wake wa kufikia malengo ya kuundwa kwake. Aidha Kamati inaishauri Wizara kuchukua juhudi za ziada za kuhakikisha ZAFICO inaongeza wigo na ubunifu ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati yangu imearifiwa kuwa, Wizara ilizalisha vifaranga vya majongoo 2,500,000 na vifaranga vya kaa 1,500,000, idadi ambayo haiendani na kile alichokiona Mhe. Makamo wa Pili wa Rais katika Ziara aliyoifanya ya kutembelea kituo cha ukuzaji wa vifaranga vya samaki – Beyt

El Ras. Aidha, Wizara imejikadiria kuzalisha vifaranga vya majongoo 2,500,000 na vifaranga vya kaa 1,500,000 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, idadi ambayo ipo sawa na takwimu ambayo Kamati iliipokea kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kamati inaitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kulitilia maanani suala hili, na kuwa makini katika kuandaa takwimu zenye ukweli na ambazo Wizara inaweza kuzifikia kiurahisi badala ya kuweka makisio yasiyokua na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imesikitishwa sana na suala zima la kuingizwa kwa samaki kutoka nje ya Nchi kwenye soko letu la ndani, ukizingatia nchi yetu ni kisiwa, tuna samaki wengi, na tuna wavuvi wabobezi na mahiri. Kamati inasisitiza kupewa kwa taaluma elekezi, vifaa na nyenzo kwa wavuvi wetu ili waweze kuvua maji marefu. Kuwezeshwa kwa wavuvi kuvua mbali kutakua na faida mbali mbali kwa serikali na jamii yetu kama ifuatavyo :-

1. Kutakua na unafuu wa bei ya samaki kwenye soko letu la ndani ikiwa samaki watavuliwa hapa hapa badala ya kuingizwa kutoka nje ya Nchi.
2. Tutaiwezesha Nchi yetu kujitosheleza kwa bidhaa ya samaki na ziada yake itauzwa kwenye masoko ya nje chini ya uratibu wa Serikali

3. Kipato cha wavuvi wetu kitaongezeka kwa asilimia kubwa sana kwasababu wataweza kuuza samaki ambao wanahitajika katika masoko ya nje
4. Uchumi wa Nchi utaongezeka kwa kupunguza uingizaji wa bidhaa kutoka nje na kuongeza usafirishaji wa bidhaa kuenda katika masoko ya nje

**Mheshimiwa Spika,**

Wavuvi wetu wanatakiwa kukata leseni za uvuvi na wanafanya hivyo, lakini leseni hiyo haitambulikani Tanzania Bara na wanakutana na changamoto kubwa sana pindi wakienda kuvua. Wavuvi wetu wanapokonywa mali zao na kubugudhiwa pindi wakiwa katika bahari za Tanzania Bara. Lakini jambo la kustaajabisha ni kuwa wavuvi wa Tanzania bara wapo huru kabisa kuja kuvua Zanzibar na leseni zao zinakubalika. Kamati yangu inaitaka Wizara kulifanyia kazi suala la kutotambulika kwa leseni ya uvuvi ya Zanzibar kule Tanzania Bara ili kuleta usawa kwa wavuvi wetu wa pande zote za Muungano na kuwafanya wavuvi wetu wavue kwa amani.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilitaarifiwa kuwepo kwa tozo ya asilimia 5-10 ya mauzo ya wavuvi kila siku ambayo inatozwa na baadhi ya

Halmashauri. Kamati inaitaka Wizara kwenda kuangalia uhalali wa tozo hizi kwani zinawaumiza sana wavuvi wetu na faida yake haionekani.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,**

Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Programu ndogo Tatu zinazojumuisha Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti na Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Uchumi wa Buluu Afisi Kuu Pemba. Aidha, Programu Kuu hii inatekelezwa na Idara ya Utawala na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Lengo la programu hii ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi na ustawi kwa sekta. Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu hii imekadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 1,773,085,000 Bilioni.

**Mheshimiwa Spika,**

Ukizingatia Lengo kuu la Serikali ya Awamu wa nane (8) la kuijenga Zanzibar mpya ya Uchumi wa Buluu, Kamati imehuzunishwa sana na uhaba wa wafanyakazi ndani ya Wizara

hii ambapo hata baadhi ya Idara hazijakamilika kimuundo. Kamati yangu ilitaarifiwa kuwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (ZPRA) ina Jumla ya Wafanyakazi 27 na Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) ina Jumla ya wafanyakazi 16. Idadi ya Wafanyakazi wa taasisi hizi mbili hairidhishi hata kidogo ukizingatia umuhimu wa taasisi hizi katika masuala mazima ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi Zanzibar. Kamati inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini, kuratibu upatikanaji wa wafanyakazi katika taasisi hizo ili kupata ufanisi katika kazi. Aidha, taasisi hizi zina uhaba mkubwa sana wa wataalamu wabobezi na Kamati ilitaarifiwa kuwepo kwa mfanyakazi ambae haripoti kazini licha ya Wizara kumgharamikia kumpeleka nje ya nchi kwa ajili ya kumpatia mafunzo ya muda mfupi ili kumuongezea ujuzi kwa ajili ya kuongeza ufanisi kazini. Kamati yangu inashauri ;-

1. Wizara ijikite sana katika kutoa mafunzo elekezi ya mara kwa mara kwa wafanyakazi wa Taasisi hizi ili kuongeza ufanisi kazini.
2. Kuyaangalia tena maslahi ya wafanyakazi wa Taasisi hizi kwani wanafanya kazi katika Taasisi nyeti na wanapaswa kuenziwa ili wafanye kazi zao kwa ufanisi mkubwa. Aidha, Kamati inahimiza suala la uzalendo kwa watumishi wa umma

kwani bila ya uzalendo na uchungu wao kwa Nchi yetu, hatutofikia malengo ya Serikali yetu katika kuleta maendeleo.

3. Kulifanyia kazi Suala la mfanyakazi aliyekataa kuripoti kazini haraka iwezekenavyo na Wizara ichukue hatua za kuliepusha tatizo kama hili kutokea tena.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuitanabahisha Wizara kwamba fedha ambazo Baraza lako Tukufu itaziidhinisha kwa Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni fedha za kodi zinazotozwa kutoka kwa Wananchi. Hivyo, Kamati yangu inaitaka Wizara kuwa makini katika matumizi itakayoyafanya ili yale malengo waliyoyapanga yaweze kutekelezwa na Wananchi nao wanufaike ipasavyo kwa mrejesho utakaofanywa kwa matumizi mazuri ya fedha zao.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara hii kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano waliotupatia wakati wa kuipitia Bajeti yao. Aidha, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu ya Uchumi imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kuipitia, kuijadili, kutoa mapendekezo yao na hatimae kuiunga mkono na kuipitisha Bajeti hii ili tumuwezeshe Waziri aende kutekeleza yale waliyojipangia katika mwaka ujao wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba ya Kamati yangu ya Uchumi, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

………………………,

Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**